

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Baruapepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Moshi*  
*16 Septemba, 2024*

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Viongozi mbalimbali. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka, Viongozi walioteuliwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Bi. Nanelwa Mwihambi ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania. Kabla ya uteuzi huu, Bi. Mwihambi alikuwa Katibu wa Bunge; na
- (ii) Bw. Baraka Ildephonc Leonard ameteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. Bw. Leonard anachukua nafasi ya Bi. Mwihambi ambaye ameteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

Viongozi walioteuliwa wataapishwa tarehe 19 Septemba, 2024 saa 09.00 alasiri, Ikulu – Dar es Salaam.

A handwritten signature in blue ink, appearing to be 'Sharifa B. Nyanga'.

Sharifa B. Nyanga  
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

